OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU

SHULE YA SEKONDARI
FLORIAN,
S.L.P 279,
KARATU
12-06-2017

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi
……

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Florian kwa mchepuo wa **CBG/CBA/HGL**.Kuchaguliwa kwake ni kutokana na kufanya vizuri katika mitihani yake ya kidato cha nne mwaka 2016.
Shule ya sekondari Florian iko katika kijiji cha **Endamarariek**,wilaya ya Karatu-mkoa wa Arusha Km 21 kutoka Karatu mjini kando ya barabara ya Karatu kwenda Mbulu.
Shule ipo katika mazingira mazuri na hali ya hewa nzuri ya mwanafunzi kusoma na kujisomea.
Kutoka Arusha mjini mpaka Karatu mjini nauli ni kati ya Tsh 5000 kwa mabasi na Hiace na Tsh 7,000 kwa usafiri wa Noah.Ila usafiri wa Noah ni wa haraka zaidi.Kwa wanaotoka mikoa ya Mara na simiyu wanaweza kutumia magari yanayopita Serengeti na watashukia Karatu Mjini .Na wanaotokea Babati,Singida na Dodoma wanaweza kushukia Makuyuni na kupanda magari yanayokwenda Karatu mjini.Upo usafiri wa Dar-es-salaam hadi karatu kwa kutumia mabasi ya Dar express na Saibaba .Nauli kutoka Karatu mjini mpaka Florian sekondari ni Tsh 2,000/= hadi 3,000/=. Ukitokea Mbulu nauli ni Tsh 5,000/= hadi kituo kinachofahamika kwa jina la Kibaoni,kutoka kibaoni haadi shuleni unaweza kutembea au kutumia usafiri wa bodaboda kwa gharama ya Tsh 1000/= tu .
Muhula wa masomo kwa mwaka huu wa 2017/2018 utaaza tarehe 03-07-2017 hivyo tunatarajia kuanza kuwapokea wanafunzi wetu Tar 02-07-2017.
Tunamkaribisha mwanao na kumtakia safari njema ya kuja Florian sekondari
KARIBU SANA

……
J.M.ISARARA
Mkuu wa shule.

Nakala
- Afisa elimu wa mkoa
  s.l.p 3032,Arusha
- Afisa elimu(w) Karatu
  s.l.p 190,Karatu
- Mwenyekiti wa BODI
  Florian Sekondari
  s.l.p 171,Karatu

ORODHA YA MAHITAJI/VIFAA AMBAVYO MWANAO ANATAKIWA KUJA NAVYO SHULENI.

S/N	AINA YA MCHANGO	KIASI/IDADI
1	Ada	**35,000** kwa muhula
2	Taaluma	**10,000** kwa muhula
3	Watumishi wasio walimu	**15,000** kwa muhula
4	Maji	**7,200** kwa muhula
5	Ukarabati	**7,500** kwa muhula
6	Michezo	**2,000** kwa muhula
7	NISHATI	**5,800** kwa muhula
8	KITAMBULISHO	**6,000** Mara moja
9	NEMBO	**2,000** Mara moja
10	TAHADHARI	**5,000** Mara moja
11	HUDUMA YA KWANZA	**5,000** Kwa muhula
	JUMLA	**100,500.00**
	MAHITAJI MENGINE	
1	Sketi damu ya mzee(deep red)kuvaa wakati usio wa masomo	**2 pieces**
2	Shati nyeupe mikono mirefu	**2pcs**
3	Sketi za shule wakati wa masomo,tunapendekeza zishonwe shuleni(Dark blue jozi mbili)	**40,000**
4	Sweta dark blue	**1pc**
5	Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufungwa kwa kamba na kisigino kifupi	**Jozi mbili**
6	Rubber (canvas) kwa ajili ya kuvaa wakati wa michezo na muda ambao sio wa masomo	**Jozi moja**
7	Soksi nyeupe(stoking)huvaliwa wakati wa masomo	**Jozi 2**
8	Nguo kwaajili ya michezo,bukta rangi yeyote,T-shirt isiyo na maandishi	**@ 1**
9	Tracksuit rangi ya darkblue yenye mistari myeupe	**Jozi 1**
10	Shuka (bed sheet)pink	**2**
11	Blanket ,mto,taulo na net	**@ 1**
12	Kikombe, bakuli, sahani na kijiko(aluminium)	**@ 1**
13	Ndoo ya lita kumi au zaidi	**1**
14	Sanduku la bati (trunker) kwaajili ya vitu vyake.	**1**
15	Ndala(slippers)	**Jozi 1**
16	Godoro 2.5ft x6ft	**1**
17	Mathematical set,daftari ,kalaamu nk	**Vya kutosha**
18	Scientific calculator kwa CBG& CBA na ya kawaida kwa HGL	**1**
19	Ream moja A4 kwa aajili ya mitihani na majaribio	**1 kwa mwaka**
20	Tochi au taa ya solar kwa dharura ya kukatika umeme	**1**
21	Kipande cha kanga	**1**
22	Jembe jipya lenye mpini CBA	**1**
23	Kwanja/slesher CBG	**1**
24	Reki kwaajili ya usafi HGL	**1**
25	t-shirt za shule zenye nembo ya sheule jozi mbili	**20,000**
25	Tai dark blue yenye mistari meupe (kwa hapa shuleni ni Tsh 4,000)	**1**
26	File cover kwaajili ya taarifa mbalimbali za mwanafunzi	**1**
27	Aje na result slip origin na photocopy(origin anaweza kurudi nayo baadae.)	

NB

- Waislamu wanaruhusiwa kushona Hijabu kwa rangi ya sare ya shule.(Angalia picha za wanafunzi)
- Mshauri binti yako asome sheria za shule kwa makini na kuzielewa.
- Mshauri kuzingatia masomo zaidi ili aweze kufaulu na kujiunga na elimu ya juu.
- Vipodozi,pafyumu,radio,kamera,simu pamoja na nguo za nyumbani haviruhusiwi shuleni.Ukaguzi utafanyika kabla yakuingia bwenini na pia utafanyika kwa dharura na akikutwa navyo bwenini hatua kali zitachukuliwa.
- Mzazi umpatie mwanao fedha za usafiri,matumizi na matibabu.
- Matibabu ni jukumu la mzazi. Mwenye bima ya afya aje nayo kwani kuna kituo cha Afya karibu na shule kinachotoa huduma kwa wenye bima. Ikumbukwe kuwa gharama za usafiri kutoka shuleni hadi kituo cha afya iwapo mwanao amezidiwa sana ni jukumu la mzazi.
- Hakikisha binti yako ajapo shuleni awe amepima afya kikamilifu,hii itatusaidia sisi kutambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu kimalezi ingawa shuleni hatuna special diet. Aidha kutakuwa na upimaji wa afya wa dharura wanafunzi wawapo shuleni.
- Fedha kwaajili ya Ada na michango mingine yote,zilipwe kwenye benki ya **NMB *Florian secondary School*.** Akaunti namba ***40901200042***, mwanafunzi aje na nakala halisi(origin) ya benki pay in slip siyo photocopy.
- Hatupokei pesa taslimu.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinga na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation).
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa .
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali ya umma.

BAADHI YA MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wezake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
vii. Uvutaji wa sigara.
viii. Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuolewa.
ix. Kupata ujauzito au kupata mimba.
x. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau bendera ya Taifa.
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

SHULE YA SEKONDARI FLORIAN

TAARIFA NA MKATABAWA UTII KWA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

1. TAARIFA (HISTORIA) YA MWANAFUNZI

   a) Jina la mwanafunzi……
      Jinsia(me/ke)…….umri……
      Mtaa/kijiji anapoishi……..

   b) Jina la mzazi/mlezi……
      Mji/kijiji/mtaa anapoishi…….
      Mawasiliano ya mzazi/mlezi
      Simu ya mkononi……. Au……(baba/mama)
      …….

2. MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI

   Mimi……naahidi kwamba sitashiriki migomo ya aina yeyote shuleni,sitafanya fujo zozoteshuleni wala kutenda kosa lolote la jinai na nakubalikutii sheria,kanuni na taratibu na maelekezo yote nitakayopewa katika muda wote nitakapokuwa shuleni.

   Jina la mwanafunzi……
   Sahihi……
   Tarehe……..

3. KUKIRI KWA MZAZI KUTOA USHIRIKIANO

   Mimi…….ambaye ni mzazi/mlezi wa …….nakiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule wakati wote atakapokuwa anasoma
   Jina…….
   Sahihi…….
   Tarehe……..

   NB fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni.